# FUNZO LA 26

1. Je, ni nani aliyempa Farao ndoto?
-Mungu.

2. Je, ndoto ya kwanza ambayo Mungu alimpa Farao ilikuwaje?
-Ng'ombe saba wembamba waliwala ng'ombe saba wanono.

3. Je, ndoto ya pili ambayo Mungu alimpa Farao ilikuwaje?
-Masuke saba membamba yalikula masuke saba yaliokuwa yamenona.

4. Je, ni nani aliyempa Yusufu kuelewa ndoto za Farao?
-Mungu.

5. Je, ndoto mbili za Farao zilimaanisha nini?
-Miaka saba ya mazao tele ingeliwa na miaka saba ya ukame.

6. Je, Mungu alitimiza vipi ndoto alizompa Yusufu, Yusufu akiwa kijana mdogo?
-Mungu alimfanya Yusufu kuwa kiongozi wa Misri yote.

7. Je, kwa nini Yakobo alichukuwa jamii yake yote kwenda Misri?
-Kwa sababu Yusufu aliishi Misri.
-Kwa sababu kulikuwa na chakula kingi Misri.

-Wakati Yakobo na wanawe na jamii zao walipohamia Misri, walikuwa sabini kwa idadi.



## Tusome Kutoka 1:1-5

1-Basi majina ya wana wa Israeli walioingia Misri ni haya; kila mtu pamoja na jamaa zake walikuja pamoja na Yakobo.
2-Reubeni, na Simeoni na Lawi, na Yuda;
3-na Isakari, na Zabuloni, na Benyamini;
4-na Dani, na Naftali, na Gadi, na Asheri.
5-Na nafsi zile zote zilizotoka viunoni mwa Yakobo zilikuwa ni nafsi sabini; na huyo Yusufu alikuwa huko ndani ya Misri tangu hapo.

-Je, jina mpya ambalo Mungu alimpa Yakobo ni lipi?
-Israeli.

-Kizazi cha Ibrahamu, Isaka na Yakobo waliitwa Israeli au Waisraeli.

-Yakobo na mwanawe Yusufu na ndugu zake na jamii zao waliishi Misri kwa miaka mingi.

-Ukame uliisha na Yusufu na ndugu zake waliendelea kuishi Misri.

-Baba yao Yakobo akafa na Yusufu na ndugu zake wakaendelea kuishi Misri.

-Baadaye, Yusufu na ndugu zake wakafa na Waisraeli wakaendelea kuishi Misri.

Tusome Kutoka 1:6

6-Yusufu akafa, na ndugu zake wote, na watu wote wa kizazi kile.

-Kwa sababu Waisraeli hawakurudi Kanaani ila waliendelea kuishi Misri, waliongezeka wakawa watu wengi.

Tusome Kutoka 1:7

7-Na wana wa Israeli walikuwa na uzazi sana, na kuongezeka mno, na kuzidi kuwa wengi, nao wakaendelea na kuongezeka nguvu; na ile nchi ilikuwa imejawa na wao.

-Baada ya miaka mingi, mfalme wa Misri, Farao, akafa.
-Kisha mfalme mpya akachukuwa mamlaka.

-Huyo Farao mpya hakuwa mkarimu kama Farao wa kwanza.
-Huyo Farao mpya alikuwa muovu sana.

Tusome Kutoka 1:8-11

8-Basi akainuka mfalme mpya kutawala Misri, asiyemjua Yusufu.
9-Akawaambia watu wake, Angalieni, watu wa wana wa Israeli ni wengi tena wana nguvu kuliko sisi.
10-Haya! Na tuwatendee kwa akili, wasije wakaongezeka; tena, ikitokea vita, wao nao wasije wakashikamana na adui zetu na kupigana nasi, na kutoka katika nchi hii.



11-Basi wakaweka wasimamizi juu yao wawatese kwa mizigo yao. Nao wakamjengea Farao miji ya kuwekea akiba, Pithomu na Ramesesi.

-Je, huyo Farao mpya aliwafanyia nini Waisraeli?
-Farao aliwafanya Waisraeli wote kuwa watumwa.

-Je, kwa nini Farao aliwafanya Waisraeli watumwa?

-Kwa sababu Farao alihofu kuwa Waisraeli wangetawala nchi yake.

-Je, kwa nini Farao alihofu kuwa Waisraeli wangetawala nchi yake?

-Kwa sababu Waisraeli waliongezeka wakawa watu wengi.

-Je, ni nani aliyekuwa akielekeza Farao kuwafanya Waisraeli watumwa?
-Shetani.

-Je, kwa nini Shetani alitaka kuwaharibu Waisraeli?

-Kwa sababu Shetani alijua kuwa Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi kupitia kwa Waisraeli.

-Shetani anamchukia Mungu.
-Shetani anawachukia watu wote.
-Shetani hakutaka Mungu amtume Mwokozi kupitia kwa Waisraeli.

-Shetani hakutaka Mwokozi aje ili awaokoe watu.

-Shetani anawachukia nyinyi nyote.
-Shetani hataki msikilize ujumbe wa Mungu.

-Shetani anawataka nyinyi nyote muelekee katika Ziwa la Moto wa Milele.

-Ingawaje Shetani alipanga kuwaharibu Israeli, Mungu aliwalinda.

-Ingawaje Shetani alipanga kuwaharibu Israeli, Mungu aliwabariki.

-Je, kwa nini Mungu aliwabariki Waisraeli?
-Kwa sababu Mungu aliwapenda Waisraeli.

-Kwa sababu Mungu hangevunja ahadi yake kwa Ibrahamu, Isaka na Yakobo.

Tusome Kutoka 1:12-14

12-Lakini kwa kadiri ya walivyowatesa ndivyo walivyoongezeka na kuzidi kuenea. Nao walichukiwa kwa sababu ya wana wa Israeli.
13-Wamisri wakawatumikisha wana wa Israeli kwa ukali;
14-wakafanya maisha yao kuwa uchungu kwa kazi ngumu; kazi ya chokaa na ya matofali, na kila namna ya kazi ya mashamba; kwa kazi zao zote walizowatumikisha kwa ukali.



-Ingawaje Farao aliwagandamiza Israeli zaidi, Mungu aliwabariki zaidi.

-Kisha siku moja, Shetani akampa Farao wazo la pili ovu.

Tusome Kutoka 1:15-22

15-Kisha mfalme wa Misri akasema na wazalisha wa Waebrania, mmoja jina lake aliitwa Shifra, na wa pili jina lake aliitwa Pua;
16-akasema, Wakati mwazalishapo wanawake wa Kiebrania na kuwaona wa katika kuzaa, ikiwa ni mtoto mwanamume, basi mwueni, bali ikiwa ni mtoto mwanamke, na aishi.
17-Lakini wale wazalisha walikuwa wakimcha Mungu, wasifanye kama walivyoamriwa na huyo mfalme wa Misri, lakini wakawahifadhi hai wale wanaume.
18-Basi mfalme wa Misri akawaita wale wazalisha na kuwauliza, Kwa nini kufanya jambo hili, na kuwahifadhi watoto waume wawe hai?
19-Wazalisha wakamwambia Farao, Ni kwa sababu hao wanawake wa Kiebrania si kama wanawake wa Kimisri; kwa sababu ni hodari hao, nao huzaa kabla mzalisha hajapata kuwafikilia.
20-Basi Mungu akawatendea mema wale wazalisha; na hao watu wakaongezeka sana, wakaendelea na kuzidi kuwa na nguvu nyingi.
21-Ilikuwa kwa sababu wale wazalisha walikuwa wakimcha Mungu, akawasimamishia nyumba.
22-Kisha huyo Farao akawaagiza watu wake, akisema,

Kila mtoto mwanamume atakayezaliwa mtamtupa mtoni, na kila mtoto mwanamke mtamhifadhi hai.

-Je, wazo la pili ovu ambalo Shetani alimpa Farao lilikuwa lipi?

-Shetani alimpa Farao wazo kuwa, wana wa kiume wa Israeli wauawe.

-Je, Mungu alijua kuwa Shetani alipanga kuwaharibu Waisraeli?
-Ndiyo.

-Je, Mungu angemruhusu Shetani kuwaharibu Waisraeli?
-La.
-Mungu aliwazingira na kuwalinda Waisraeli.

-Mungu pia alipanga kuwaondoa Waisraeli kutoka Misri na kuwarejesha Kanaani.

-Mungu alipanga kuwaondoa Waisraeli kutoka Misri kurejea Kanaani kupitia kwa mtu mmoja aitwaye Musa.

-Ifuatayo ni hadithi ya Musa:

Tusome Kutoka 2:1-4

1-Mtu mmoja wa nyumba ya Lawi akaondoka akaoa binti mmoja wa Lawi.
2-Yule mwanamke akachukua mimba akazaa mwana, na alipoona ya kuwa ni mtoto mzuri akamficha miezi mitatu.



3-Na alipokuwa hawezi kumficha tena, akampatia kisafina cha manyasi akakipaka sifa na lami, akamtia mtoto ndani yake, akakiweka katika majani kando ya mto.
4-Umbu lake mtoto akasimama mbali ili ajue yatakayompata.

-Wazazi wa Musa walimwamini Mungu.

-Wazazi wa Musa waliamini kuwa Mungu angemlinda mwana wao.

-Kwa hivyo Mungu akawapa wazo la kumweka Musa katika kikapu na kukiweka kile kikapu katika mto Nilo.

-Je, Mungu alimlinda mwanao Musa?

Tusome Kutoka 2:5-10

5-Basi binti Farao akashuka, aoge mtoni, na vijakazi wake wakatembea kando ya mto; naye akakiona kile kisafina katika majani, akamtuma kijakazi wake kwenda kukileta.
6-Akakifungua, akamwona mtoto, na tazama, mtoto yule analia. Basi akamhurumia, akasema, Huyu ni mmojawapo wa watoto wa Waebrania.
7-Basi umbu lake mtoto akamwambia binti Farao, Je! Niende nikamwite mlezi katika wanawake wa Kiebrania, aje kwako, akunyonyeshee mtoto huyu?
8-Binti Farao akamwambia, Haya! Enenda. Yule kijana akaenda akamwita mama yake yule mtoto.
9-Binti Farao akamwambia, Mchukue mtoto huyu,

ukaninyonyeshee, nami nitakupa mshahara wako. Yule mwanamke akamtwaa mtoto, akamnyonyesha.

10-Mtoto akakua, naye akamleta kwa binti Farao, akawa mwanawe. Akamwita jina lake Musa, akasema, Ni kwa sababu nalimtoa majini.

-Mungu alimtuma binti ya yule Farao mwovu kumlinda Musa.
-Mungu alimtuma binti ya yule Farao mwovu kuwa mlezi wa Musa.

-Na Musa akaishi na yule Farao mwovu na binti yake.

-Je, kwa nini Mungu alimtuma binti ya Farao kumwokoa Musa?

-Kwa sababu Mungu alipanga kuwaongoza Israeli kutoka Misri kupitia kwa Musa.

-Kwa sababu Mungu alipanga kuwaongoza Waisraeli kutoka utumwani kupitia kwa Musa.

-Mungu alijua kuwa Musa angekuwa salama katika nyumba ya Farao.

-Mungu alijua kuwa Musa angejifundisha kusoma na kuaandika katika nyumba ya Farao.

-Mungu alijua kuwa Musa angejifundisha mambo mengi ambayo yangemsaidia kuwaongoza Waisraeli.



-Farao alipanga kuwaharibu Waisraeli, lakini Mungu aliwalinda Waisraeli.

-Shetani na mapepo wake walipanga kuwaharibu Waisraeli, lakini Mungu aliwalinda.

-Je, kuna yeyote anayeweza kuzuia kazi ya Mungu?
-La.

-Je, pepo yeyote anaweza kuzuia kazi ya Mungu?
-La.
-Je, Shetani anaweza zuia kazi ya Mungu?
-La.

-Mungu ni mwenye nguvu zote.

-Mungu aliwalinda Israeli na atamlinda yeyote anayemwamini.

-Musa alikuwa katika nyumba ya Farao na akawa mtu mzima.

-Siku moja, Musa alienda kuona jinsi Waisraeli walivyokuwa wakiteseka katika utumwa.

Tusome Kutoka 2:11-14

11-Hata siku zile, Musa alipokuwa mtu mzima, akatoka kuwaendea ndugu zake, akatazama mizigo yao. Akamwona Mmisri anampiga Mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake.
12-Basi akatazama huko na huko, na alipoona ya kuwa hapana mtu, akampiga Mmisri yule, akamficha ndani ya

mchanga.

13-Akatoka siku ya pili, na tazama, watu wawili wa Waebrania walikuwa wakipigana. Akamwambia yule aliyemdhulumu mwenzake, Mbona unampiga mwenzako?

14-Yule akasema, Ni nani aliyekuweka wewe kuwa mkuu wetu, na mwamuzi juu yetu? Je! Wataka kuniua mimi kama ulivyomwua yule Mmisri? Musa akaogopa, akasema, Kumbe! Jambo lile limejulikana.

-Je, Waisraeli wangeweza kujiokoa kutoka kwa Farao?
-La.

-Musa alijaribu kuwaokoa Waisraeli, na alimuua Mmisri mmoja.

-Lakini Farao aligundua kuwa Musa alimuua Mmisri.

-Je, Farao alifanya nini?

Tusome Kutoka 2:15

15-Basi Farao alipopata habari, akataka kumwua Musa; lakini Musa akakimbia mbele ya Farao, akakaa katika nchi ya Midiani; akaketi karibu na kisima.

-Farao aligundua kuwa Musa alimuua Mmisri.
-Kwa hivyo Farao alijaribu kumuua Musa.

-Musa aliogopa na akatoroka.
-Musa alitorokea nchi ya Midiani.



-Je, Musa aliweza kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa Farao?
-La.

-Musa alijaribu kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa Farao lakini hakuweza.

-Je, ni nani pekee aliyeweza kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa Farao?
-Mungu.

-Je, ni nani pekee awezaye kuwaokoa watu kutoka kwa Shetani?
-Mungu.

-Kama vile Waisraeli walivyokuwa mateka wa Farao, ndivyo watu wote huwa mateka wa Shetani.

-Kama vile Waisraeli hawangeweza kujiokoa kutoka kwa Farao, ndivyo watu wote wasivyoweza kujiokoa kutoka kwa Shetani.

-Kama vile Musa hangeweza kuwaokoa Waisareli kutoka kwa Farao, basi hakuna anayeweza kujiokoa kutoka kwa Shetani.

-Kama vile ni Mungu pekee aliyeweza kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa Farao, hivyo basi ni Mungu pekee awazaye kutuokoa kutoka kwa Shetani.

-Katika fundisho linalofuata, tutajifundisha mengi kumhusu Musa.